Toleo 89 - Dhu al-Qi’dah 1445 H / Juni 2024 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Vibaraka wa Makafiri wa Magharibi na Ukakamavu wa Kuendelea na Mradi wa Kuigawanya Sudan

**HABARI NA MAONI**
Uoga ni Fedheha, Ilhali Katika Kumkabili Adui Kuna Heshima

**MATOLEO**
Barakoa Zimepomoka: Miaka 76 ya Ukaliaji Kimabavu wa Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina

**JIBU LA SWALI**
Kuzungumza Neno la Haki kwa Sauti Kubwa




## Mpaka Lini, Enyi Ummah wa Muhammad?!

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari
Wilayah Sudan

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 44/1445 | Jumapili, 11 Dhu al-Qi'dah 1445 H | 19/05/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Vibaraka wa Makafiri wa Magharibi na Ukakamavu wa Kuendelea na Mradi wa Kuigawanya Sudan

Abdul Wahid Nur, kiongozi wa Vuguvugu la Ukombozi wa Sudan, na Waziri Mkuu wa zamani Abdalla Hamdok walitia saini tangazo jijini Nairobi, mji mkuu wa Kenya. Mojawapo ya vifungu vyake muhimu zaidi ni pamoja na: Kifungu cha 4, nukta (d), ambacho kinataka kuanzishwa kwa serikali kisekula ambayo itasalia kutoegemea upande wowote na iliyo ya kati na kati kidini, kitamaduni na vitambulisho vyote. Nukta (e) inataka kuanzishwa kwa serikali ya majimbo ya kiraia ya kidemokrasia nchini Sudan ambayo inahakikisha kuundwa kwa serikali ya kiraia. Pia inajumuisha vipengee vya uhuru wa dini na fikra, na inadhamini utambulisho wa kitamaduni, kikabila, kidini na kikanda. Tangazo hilo linahitimisha kifungu hiki kwa kusema: "Ikitokea kwamba kanuni hizi hazijajumuishwa katika katiba ya kudumu, watu wa Sudan wana haki ya kujiamulia wenyewe."

**Kwa kuzingatia tangazo hili, sisi katika Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan tunathibitisha ukweli ufuatao:**

**Kwanza:** Sudan imetawaliwa na mfumo wa kisekula tangu kuingia kwa majeshi ya wakoloni wa Uingereza mwaka 1899 hadi leo, ambapo katiba ilianzisha maisha kwa msingi wa kutenganisha Dini na maisha.

**Pili:** Sababu ya msingi ya matatizo yote ya Sudan ni fikra ya usekula, au demokrasia, ambayo ni wazo moja linalomaanisha utekelezaji sheria zilizotungwa na binadamu kupitia mabunge na mabaraza ya kutunga sheria, na kutengwa kwa hukmu ya Muumba, Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Tatu:** Msisitizo wa viongozi hawa, wawe wanasiasa au wanajeshi, katika kutabikisha usekula unalenga kutekeleza maamrisho na maagizo ya dola za kikoloni zinazojitahidi kuupiga vita Uislamu na kuuzuia kutawala na siasa, hivyo kupambana na wabebaji na watetezi wake.

**Nne:** Kuanzisha maisha juu ya itikadi ya kutenganisha Dini na dola kunamaanisha kuendelea na maisha ya shida, mateso, na kufeli katika kusimamia nyanja zote za maisha, iwe ya kisiasa au ya kiuchumi. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

وَمَنْ أَعْرَضَ عَنْ ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكاً وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى

**"Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu."** [Taha:124].

**Tano:** Kufanya kazi ili kutabikisha majimbo, kujitawala wenyewe, na kujiamulia wenyewe ni kuiweka nchi katika mashini ya ugawanyaji na uharibifu, na ni kazi chafu inayotekelezwa tu na vibaraka walioanguka.

**Kwa kumalizia:** Tangazo hili linathibitisha jinsi vibaraka wa dola za kikoloni wanavyofanya njama usiku na mchana kutekeleza mpango wa mabwana zao nchini Sudan, ambao unazunguka pembetatu ovu: ukiondoa Uislamu na kupigana na wabebaji na watetezi wake kwa kuweka ubaguzi wa kidini, kuigawanya Sudan kupitia majimbo, kujitawala wenyewe, na kujiamulia wenyewe, na kisha kupora rasilimali kupitia wawekezaji wa kigeni na makampuni ya kibepari ya kikoloni.

Wajibu wa watu wa Sudan ni kuchukua msimamo dhidi ya viongozi hawa wasaliti, kuwafichua, na kusimamisha Dola ya Kiislamu; Khilafah Rashida kwa njia ya Utume. Hili litaunganisha Ummah chini ya kitambulisho cha Uislamu, licha ya tofauti za rangi na lugha, ambapo hakuna aliye mbora kuliko mwengine isipokuwa kwa taqwa (uchamungu). Kupitia bayah (ahadi ya utiifu) halali kwa Khalifa ambaye anasimamia uadilifu, anayehakikisha usalama, na anayempa kila mtu haki yake inayostahiki.

[وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنصُرُ مَن يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ]

**"Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu."** [Ar-Rum:5]

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir katika Wilayah Sudan**

# Barakoa Zimepomoka: Miaka 76 ya Ukaliaji Kimabavu wa Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na Maryam Ansari**



Jarida la 'Economist' liliripoti mnamo Mei 14, 2024 kwamba, "Uwashaji wa mwenge ambao kwa kawaida hufungua Siku ya Uhuru wa "Israel" ulitangazwa mnamo jioni ya Mei 13 kama kawaida. Lakini badala ya kuonyeshwa moja kwa moja kwenye televisheni kama kawaida, hafla hiyo ilirekodiwa mapema. Serikali ilisema hii ni kwa sababu ya hali tete ya kufanya sherehe hiyo wakati taifa liko vitani. Sababu halisi, hata hivyo, ilikuwa hofu ya wanasiasa kwamba ingevurugwa na waandamanaji, waliokasirishwa na kufeli kwao katika kushughulikia vita."

Ingawa umbile la Kiyahudi liko katika msukosuko wa ndani leo, uanzishwaji wake wa asili ni utengezaji ambao ulidunga moyo wa Ulimwengu wa Kiislamu. Damu ilimwagika katika nchi takatifu kama ilivyokuwa wakati wa vita vya msalaba vya karne ya 11. Kuzaliwa kwake kuliwezekana tu kwa kufukuzwa kwa lazima kwa watu ambao walikuwa tayari wanaishi huko na usaliti wa watawala wa Kiarabu katika eneo hilo. Waislamu na Wakristo ambao walikuwa wameishi huko kwa karne nyingi walifukuzwa na magenge ya kigaidi ya Kizayuni, katika kile kinachojulikana kama Nakba, janga. Waislamu na Wakristo walifukuzwa katika nyumba zao, vijiji vilichomwa moto, na wanaume, wanawake na watoto wasio na hatia walichinjwa na walowezi wa Kizayuni, waliokuja kutoka Ulaya kudai ardhi hiyo kuwa ni yao. Maelfu ya Mayahudi kutoka duniani kote walipewa ardhi ambayo ni mali ya wengine. Palestina ikawa mahali pa ukaliwaji kimabavu. Wapalestina waliolazimishwa kuondoka hawajawahi kuruhusiwa kuregea.

**Barakoa ya uvamizi wa kikatili wa Wazayuni, unaoungwa mkono na Marekani, imepomoka.** Marekani iliwapa nguvu Wazayuni na kufumbia macho yote waliyoyafanya. Marekani ilitumia uwezo wake wa kura ya turufu katika Umoja wa Mataifa kuwakinga Wazayuni dhidi ya vikwazo vyovyote au adhabu kutoka kwa jumuiya ya kimataifa. Kwa muda wa miaka 76, Wazayuni wameendelea kunyakua ardhi na kueneza ugaidi, wakifanya mamia ya vizuizi na kuzuia maisha ya utulivu kwa Wapalestina. Miaka sabiini na sita baadaye, mabadiliko pekee katika Palestina inayokaliwa kwa mabavu ni teknolojia ya hali ya juu yenye kulipua nyumba, shule na hospitali. Uhalifu usioelezeka, kama vile makaburi ya halaiki yaliyofichuliwa kwenye misingi ya hospitali baada ya wiki kadhaa za uvamizi wa Wazayuni. Kuhama kwa lazima, njaa ya kulazimishwa, na kuporomoka kabisa kwa miundo ya jamii inayofanya kazi kumesababisha hali ya kutisha zaidi huko Gaza. Kwa muda wa miezi saba, tumeona mauaji ya halaiki yakitokea mbele ya macho yetu. Inatupa taswira ya ukandamizaji wa Wapalestina katika kipindi cha miaka 76 iliyopita.

Sura mbaya, isiyofichika ya uvamizi huo wa kikatili sasa imeuamsha Ummah. Uvamizi wa hapo awali wa jeshi la Kizayuni huko Gaza ulikuwa habari za muda mfupi. Lakini wakati huu, ni tofauti. Safari hii Waislamu wameamka. Kutoka Morocco hadi Malaysia, Umma wa Kiislamu unahamasishwa na kusonga mbele. Nguzo za kirongo za Magharibi zimeanguka. Waislamu hawana matumaini katika suluhisho la Magharibi kwa Palestina. Unafiki unadhihirika. Mikono iliyolowa damu ya Marekani na dola za Ulaya haiwezi kufichwa.

**Barakoa za taasisi za wakoloni wa Magharibi zimepomoka.** Umoja wa Mataifa, Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC) hutumikia maslahi ya Marekani. Umoja wa Mataifa, ulioundwa na Marekani mwaka 1945, ulionyeshwa kama chombo kisichoegemea upande wowote kilichoundwa kulinda watu wote na kuzuia vita vyote. 'Never again' ndiyo iliyokuwa kauli mbiu. Ilidaiwa kuwa kamwe hataruhusiwa tena mtu yeyote kuwaua watu wengi kutokana na kabila au dini. Lakini ilikuwa ni Umoja wa Mataifa uliokuwa skrini ambayo nyuma yake kulikuwa na mpango wa kuwaibia Ummah wa Kiislamu Qibla chao cha kwanza. Mpango ambao ulibuniwa kumpumbaza mtu wa kawaida kufikiri kwamba ni suala la muda tu kabla ya amani kupatikana na Waislamu, Wakristo, na Mayahudi wataishi bega kwa bega. Wahusika wa tamthilia hii tata walikuwa ni

***Endelea... UK 4***

wale walioitwa wapenda amani wa Magharibi ambao wangeleta pande tofauti pamoja. Wachezaji wa pembeni walikuwa ni watawala wa Waislamu walioamriwa kujilinda kama vibaraka viziwi na mabubu, kusema tu wanapozungumzishwa na kusema tu kile ambacho maandishi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani iliwaambia waseme.

Maazimio na makubaliano mengi ya Umoja wa Mataifa yametiwa saini kuhusu ukiukaji wa sheria za Kimataifa wa dola ya Kizayuni huko Palestina. Bado wameshindwa kusuluhisha uvamizi na ukandamizaji mkali wanaopitia Waislamu wa Palestina. Badala yake, wamezidisha hali na hali ya wale wanaoishi katika Ardhi hii Iliyobarikiwa. Wamerefusha muda wa uvamizi. Maazimio yasiyo na maana yaliyopendekezwa na Umoja wa Mataifa kulaani kitendo cha kikatili cha "Israel" yalikataliwa na Marekani, kupitia kura yake ya turufu. Yale yaliyopitishwa yalivunjwa na Wazayuni, bila matokeo yoyote. Kwa hivyo, barakoa ya UN imepomoka. Iliundwa na Marekani kutumikia maslahi yake.

Kadhia ya Palestina kamwe haiwezi kutatuliwa na shirika la makafiri kama UN au makafiri waliovalia suti na tai zao wakiwa wanaonyesha tabasamu za uongo. Hakuwezi kuwa na binadamu mwenye akili timamu ambaye bado angetetea kukabidhi kadhia hii kwa Umoja wa Mataifa kutafuta suluhu. Zaidi ya hayo, Qur'an Tukufu ilituonya miaka 1400 iliyopita ili tujue ni nani alikuwa adui yetu na tusidanganywe nao. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ ٱلْكَـٰفِرِينَ أَوْلِيَآءَ مِن دُونِ ٱلْمُؤْمِنِينَ ۚ أَتُرِيدُونَ أَن تَجْعَلُواْ لِلَّهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَـٰنًا مُّبِينًا

**"Enyi mlio amini! Msiwafanye makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je, mnataka Mwenyezi Mungu awe na hoja iliyo wazi juu yenu?"** [Surah An-Nisa 4: 144].

Barakoa za watawala wa Waislamu zimepomoka. Wanaendelea kukataa kutuma majeshi ya Waislamu kukomesha mauaji ya halaiki nchini Palestina. Erdogan anaendelea kusambaza silaha, vifaa, na chakula kinachohitajika kuendeleza mauaji ya halaiki. Misri, chini ya dikteta katili Al-Sisi, inafunga Kivuko cha Mpakani cha Rafah. Abdallah wa Jordan anatoa daraja la anga, pamoja na ukanda wa ardhini pamoja na Saudia na Imarati, ili kusafirisha vifaa vya kijeshi vya Marekani kwa Wazayuni. Watawala wa Waislamu wanaoizunguka Palestina ni watetezi wa Wazayuni pekee. Wamewafunga na kuwatesa walioandamana kupinga mauaji ya halaiki. Viongozi wote 57 wa nchi za Waislamu wanashiriki katika mauaji ya halaiki kupitia kukataa kwao kupeleka majeshi. Wana uwezo zaidi wa kuwaponda Wazayuni, lakini wanachagua kuwatumikia mabwana zao. Ni kana kwamba hawakusikia maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw).

مَا مِنْ امْرِئٍ يَخْذُلُ امْرَأً مُسْلِماً فِي مَوْضِعٍ تُنْتَهَكُ فِيهِ حُرْمَتُهُ وَيُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ إِلَّا خَذَلَهُ اللهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ فِيهِ نُصْرَتَهُ، وَمَا مِنْ امْرِئٍ يَنْصُرُ مُسْلِماً فِي مَوْضِعٍ يُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ وَيُنْتَهَكُ فِيهِ مِنْ حُرْمَتِهِ إِلَّا نَصَرَهُ اللهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ نُصْرَتَهُ

**"Hakuna (Muislamu) mtu yeyote atakayemtelekeza Muislamu katika sehemu ambayo utukufu wake unakiukwa na heshima yake inavunjwa isipokuwa Mwenyezi Mungu atamtelekeza katika sehemu ambayo angependa nusra Yake. Hakuna (Muislamu) mtu yeyote atakayemnusuru Muislamu katika sehemu ambayo heshima yake inavunjwa utukufu wake unakiukwa isipokuwa Mwenyezi Mungu atamnusuru katika sehemu ambayo angependa nusra Yake."** [Abu Daud]

Kabla ya watawala wa sasa, kwa miaka 1300, Khilafah ilikuwa imeilinda na kuihami Ardhi Iliyobarikiwa. Khilafah ya Umar al-Farooq (ra) iliifungua Palestina kwa Uislamu. Khilafah ilituma vikosi vya Salahudin kwenda kuikomboa kutoka kwa makruseda. Khilafah ya Abdul Hamid II iliilinda Palestina kutokana na majaribio ya Wazayuni ya kupora ardhi yake. Kwa kukosekana Khilafah, Palestina imebakia chini ya uvamizi.

**Barakoa zote zimepomoka.** Viongozi wa Magharibi na mfumo wao batili wa maisha wamefichuliwa. Taasisi na mahakama zao zimefichuliwa. Khiyana ya watawala wa Waislamu umefichuliwa. Washawishi na watu mashuhuri wamefichuliwa. Waliokaa kimya wamefichuliwa. Hatuwezi kuwa na tumaini lolote kwa yeyote kati yao. Kufanya hivyo itakuwa ni kukataa uhalisia. Mujahidina wa kweli wametimiza ahadi yao na Mwenyezi Mungu (swt). Wanaume, wanawake, watoto wadogo na wachanga ambao hawajazaliwa huko Gaza wametimiza ahadi yao na Mwenyezi Mungu (swt). Sisi tunafanya nini ndugu zangu na dada zangu? Mitandao ya kijamii na maandamano lazima yatumike kulingania suluhisho sahihi.

Palestina haitakombolewa kwa kujifunza kuhusu historia yake. Kususia, kutengwa na vikwazo havitaikomboa Palestina. Palestina haitakombolewa kwa msaada wa chakula. Palestina itakombolewa wakati wana shupavu wa Umma katika majeshi ya Waislamu watakapowaasi watawala wasaliti, wakavunja minyororo yao na kuandamana kuelekea Al Quds. Suluhisho la Palestina ni kupeleka majeshi yetu ya Waislamu Aqsa. Suluhisho la Palestina ni kwa maafisa shupavu wa Ummah kuwang'oa watawala na kutoa Nusrah kwa ajili ya kusimamisha Khilafah Rashida. Ni Khilafah ndiyo itakayoikomboa Palestina na Al Aqsa. Dori yetu ni kuyataka majeshi yaende kuulinda Ummah. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِن تَنصُرُواْ ٱللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

**"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu."** [Surah Muhammad 47:7].

# Mpaka Lini, Enyi Ummah wa Muhammad?!



Uharibifu na kukatwa vipande vipande, kulipuliwa kwa mabomu na mauaji makubwa, kunajisiwa Msikiti wa Al-Aqsa na kumtukana Mtume (saw) ndani ya nyua zake. Hivi, mpaka lini, enyi Umma wa Muhammad (saw)?!

Kwa muda wa miezi saba tumekuwa tukiulingania Ummah wetu na majeshi yake kwa ajili ya jihad kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tukiwalingania kwa wito wa Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرَضِيتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ * إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَاباً أَلِيماً وَيَسْتَبْدِلْ قَوْماً غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئاً وَاللهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**“Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache. Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”** [At-Tawba:38-39]. Hivi, mpaka lini, enyi Ummah wa Islam?!

Je, sio wakati wa nyinyi kuzipindua tawala za khiyana na watawala vibaraka? Je, maneno yao matupu hayakukasirishi, ambayo kwayo wanamwita adui wa Kiyahudi kuzingatia sheria na maazimio ya kimataifa? Je, ni sheria na maazimio gani wasaliti hawa wanazozungumzia? Kwa muda wa miezi saba wale waliokasirikiwa na Mwenyezi Mungu (Mayahudi) wamekuwa wakiwaua watoto, wanawake, wagonjwa na wafungwa, wakiharibu hospitali, misikiti na taasisi za elimu. Wamelenga hata mashirika ya kimataifa ya kutoa misaada, wakiua wanachama wao na kuharibu makao yao makuu. Ni kipi kimesalia kutoka kwa sheria za kimataifa ambacho hawajakiuka? Ni matukufu gani yanayobakia ambayo hawajayachafua?

**Enyi Umma wa Muhammad (saw):** Damu yetu inamwagwa kwa kiasi kikubwa, na kwa upande wake, Marekani na vibaraka wake wanazungumza kuhusu misaada ya kibinadamu, suluhisho la dola mbili, na uhalalishaji mahusinao na wale waliokasirikiwa na Mwenyezi Mungu. Je, kuna uhalifu mkubwa kuliko huu?! Wanatuma misaada pamoja na mabomu ya kifo, wanazungumza kuhusu amani na uhalalishaji mahusiano huku wakiendelea na mauaji na uharibifu wao. Na sasa, kundi la wasaliti la watawala vibaraka nchini Misri, Jordan, Qatar, na ardhi ya Misikiti Miwili Mitakatifu

***Endelea... UK 6***

wanashirikiana na Marekani kwa ajili ya mipangilio ya baada ya vita, mipangilio hiyo inayolenga kurekebisha sura ya dola halifu na inayokalia kimabavu, kuiunganisha katika eneo hilo, na kuzima kadhia ya Palestina.

**Enyi Waislamu:** Uthabiti na ushujaa wa mujahidina unakulazimuni kuwanusuru kikweli, na hivyo kupelekea kukombolewa kwa Ardhi Iliyobarikiwa na Msikiti wa Al-Aqsa. Hata hivyo, watawala vibaraka na mashirika yao ya kijasusi wanafanya kazi kwa nguvu zao zote kubadilisha ushujaa wa mujahidina na damu na mateso kuwa kushindwa kukubwa kuliko kule kwa 1948 na kikwazo kibaya zaidi kuliko kile cha 1967. Ushujaa wa jeshi la Misri katika Ramadhan 1973 ilihujumiwa na makubaliano ya amani ya khiyana yaliyotiwa saini na Sadat, ambayo watu wa Misri na Palestina bado wanateseka nayo.

Kile ambacho Marekani, Mayahudi na watawala vibaraka wanapanga dhidi ya watu wa Palestina ni njama kubwa. Vipaumbele vyao vya sasa ni kuwaondoa mujahidina na hamasa ya jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu, na kuanzisha mamlaka katika Gaza ambayo inayofanya uratibu pamoja na Uvamizi sawa na chombo cha Mamlaka ya Palestina mjini Ramallah. Wale waliopata ghadhabu ya Mwenyezi Mungu wanapiga dau juu ya fursa, na uhalisia wao umeelezwa katika maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

أَمْ لَهُمْ نَصِيبٌ مِنَ الْمُلْكِ فَإِذاً لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيراً **"Au wanayo sehemu ya utawala? Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende."** [An-Nisa:53]. Wanataka Palestina yote, na macho yao yatulizwa kwenye ardhi vilevile. Ama kuhusu mradi wa Marekani wa suluhisho la dola mbili, umekosa maana.

**Enyi Umma wa Muhammad (saw):** Matukio ya Gaza yameamsha fahamu ya ukombozi na faradhi ya jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu, na kujenga hisia ya jumla kwa Waislamu kwamba ukombozi wa Masra ya Mtume (saw) uko karibu zaidi kuliko wakati mwengine wowote. Hata hivyo, Marekani na watawala vibaraka wanataka kuupotoa Umma wa Kiislamu kutoka katika ukombozi na jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa kupigia debe suluhisho la dola mbili na kuuonyesha Umma wa Kiislamu kuwa ni dhaifu na usio na nguvu, ambao lazima ujisalimishe na kusalimu amri kwa matakwa ya Marekani na umbile la Kiyahudi.

Usaliti wa tawala hizo utawatumbukiza Waislamu katika dimbwi la njama, udhalilifu na ukandamizaji. Hili linawalazimu Waislamu kwa jumla na hasa majeshi kufanya kazi kwa nguvu zao zote ili kujinasua kutoka katika utegemezi na uwakala, kuzipindua tawala, kuondoa mipaka ya Sykes-Picot, na kusimamisha hukmu ya Mwenyezi Mungu duniani.

Ewe Umma Bora ulioletwa kwa ajili ya wanadamu: Jukumu la Umma wa Kiislamu kwa ulimwengu ni kubwa sana. Inaulazimu Ummah kusimama kwa ajili ya Dini yake kama alivyokusudia Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuwa shahidi kwa watu, shahidi kwao ukisimamisha Dini na kupiga vita dhulma na jeuri.

Hakika ni wakati wa sisi kuwaokoa wanadamu kutoka kwa dhulma hii halifu ya kibepari. Harakati ya uhamasishaji inayoshuhudiwa hivi sasa ulimwenguni ni ishara ya matumaini kwa wanadamu wote. Wanafunzi hawa walikua wakitukuza uhuru na kuuzingatia kuwa ni dhihirisho la ukuu wa Marekani, lakini sasa wako kwenye mgongano na dola yenye jukumu la kutabikisha mfumo na kudhamini haki yao ya kujieleza. Kukandamiza na kutawanya kwa nguvu vikao ni pigo kwa kanuni msingi za mfumo wa kibepari, na huu ni utangulizi wa kuporomoka kwa Marekani na mifumo ya Kimagharibi.

Muungano wa Kisovieti uliporomoka pale imani katika mfumo wa Kikomunisti na fahamu zake za kimsingi za maisha ilipopotea, na Khilafah iliporomoka pale fahamu za kimsingi za Waislamu zilipopotoshwa, na kusababisha Uislamu kupoteza ushawishi wake kwa serikali na jamii. Hiki ndicho kinachotokea Magharibi sasa. Kinachotokea sio tu kukandamiza uhuru wa mtu binafsi wa kujieleza bali **ukandamizaji wa fikra hiyo katika jamii**. Haya ni matokeo yasiyoweza kuepukika ya kupoteza imani katika demokrasia kama njia ya maisha na kupoteza imani katika mfumo wa kidemokrasia unaotawala.

Mtegemeeni Mwenyezi Mungu Al-Qawii Al-Aziz na mufanye kazi kwa bidii pamoja na Hizb ut Tahrir ili kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu duniani. Mwenyezi Mungu (swt) ataleta nusrah (ushindi) yake kupitia mikono yenu kwa uwezo wake usioshindika.

إِنْ يَنْصُرْكُمُ اللهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمْ وَإِنْ يَخْذُلْكُمْ فَمَنْ ذَا الَّذِي يَنْصُرُكُمْ مِنْ بَعْدِهِ وَعَلَى اللهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

**"Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindeni, na akikutupeni ni nani, basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu."** [Aal-i-Imran:160]

**Ewe Mwenyezi Mungu, zifungue nyoyo za Waislamu kwenye utiifu Wako, radhi Zako, na nusra ya Dini Yako. Tujaaliye kutoka Kwako mamlaka yenye kunusuru. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.**

**H. 5 Dhu al-Qi'dah 1445** **Hizb-ut-Tahrir**
**M. : Jumapili, 05 Mei 2024** **Ardhi ya Baraka-Palestina**

# HABARI NA MAONI

# Uoga ni Fedheha, Ilhali Katika Kumkabili Adui Kuna Heshima

**Habari:**

Gazeti la ‘Express Tribune’ la Pakistan liliripoti mnamo tarehe 1 Mei 2024 kwamba, "Pakistan, China na Iran hivi karibuni zitafanya mkutano wa pande tatu juu ya kukabiliana na ugaidi na usalama katika ishara nyingine ya kukua kwa dori ya Beijing, kuwaleta pamoja majirani katika masuala muhimu. Mkutano wa kwanza wa Mashauriano ya pande tatu za Pakistan-China-Iran kuhusu kukabiliana na ugaidi na usalama ulifanyika jijini Beijing mwezi Juni mwaka jana." [Tribune]

**Maoni:**

Iran na Pakistan zilikutana pamoja na China kwa ajili ya nini mnamo Juni 2023? Je, wanakusudia kukutana tena na China kwa ajili ya nini? Kushirikiana katika kukabiliana na ugaidi! Kushirikiana na gaidi China, ambayo inawapiga vita Waislamu huko Xinjiang na Dini yao! Kushirikiana na dola adui, huku ikiipa Dola ya Kibaniani uhuru juu ya Kashmir Inayokaliwa kimabavu, na umbile la Kiyahudi uhuru juu ya Palestina! Mkutano huu haungeweza kuwa mbaya na wa kuchukiza zaidi hivi, kwani unajiri katika wakati ambapo kina dada na watoto wetu wanauawa na magaidi halisi wa zama zetu.

Ilhali, serikali za nchi mbili kubwa za Waislamu zitakutana tena kuhusiana na ugaidi, wakati ambapo umbile la Kiyahudi limeendesha zaidi ya siku mia mbili za ugaidi kwenye Ardhi Iliyobarikiwa ya Masjid Al-Aqsa. Zaidi ya watu 34,000 wameuawa shahidi na uvamizi wa Kiyahudi, kwa kutumia silaha na mifumo ya silaha kutoka nchi za Magharibi. Kupoteza maisha ni kando na uharibifu wa karibu miundombinu na makaazi yote. Tangazo la serikali zenye majeshi mawili yenye nguvu zaidi ya Kiislamu, katika wakati kama huo wa kuhuzunisha moyo kwa Umma, ambalo sio la kutangaza uhamasishaji wa majeshi kukomesha ugaidi wa Kizayuni, ni usaliti kwa matukufu ya Uislamu.

Amri kwa askari mashujaa wa Uislamu, na mifumo ya silaha katika matumizi yao si chochote ila ni neema ya Mwenyezi Mungu, Al-Aziz Al-Mutakabbir. Kabla ya vita vya Mu’tah, habari ziliwafikia askari 3000 wa Kiislamu kwamba Hiraqla alikuwa amekusanya askari laki moja kwa pamoja, pamoja na askari wengine laki moja wa Lakham, Judham na Balqain, makabila ya Waarabu yanayoungana na Wabizantini. 'Abdullah bin Rawaha aliwahutubia Waislamu kwa  kusema, وما نقاتل الناس بعدد ولا قوة ولا كثرة، ما نقاتلهم إلا بهذا الدين الذي أكرمنا الله به، فانطلقوا، فإنما هي إحدي الحسنيين، إما ظهور وإما شهادة “Katika pambano letu hatutegemei idadi ya askari au zana bali juu ya Dini ambayo Mwenyezi Mungu ametukirimu kwayo. Jitahidini kushinda mojawapo ya hayo mawili, ushindi au shahada.” Imepokewa na Al-Bukhari kwamba Khalid bin Waleed, Upanga wa Mwenyezi Mungu, alitumia panga tisa ambazo zilivunjika wakati alipokuwa akipambana na maadui wa Uislamu bila kuchoka na kwa ujasiri. Hakika amri ya askari wa Kiislamu inafananishwa na upanga wa Mwenyezi Mungu. Inawajibisha kwamba silaha zitumike kwa utukufu wa Neno la Mwenyezi Mungu (swt). Inawajibisha kwamba silaha hizo zitumike na watu ambao wana imani kamili katika ushindi (Nasr) ya Mwenyezi Mungu (swt).

Kuhusu silaha za Waislamu, kumbukeni tukio la kabla ya Vita vya Uhud pale Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alipochukua upanga mkali, akaushika mkononi mwake na akawaita Maswahaba zake na kusema, **من يأخذ هذا السيف بحقه؟** **“Ni nani aliye tayari kuchukua upanga huu na kuupa haki yake inayostahili?”** Wanaume wengi walikuwa tayari kuuchukua. Baadhi yao walikuwa ni ‘Ali bin Abi Talib, Az-Zubair bin Al-‘Awwam na ‘Umar bin Al-Khattab. Lakini haikupewa yeyote. Abu Dujana Sammak bin Kharsha akauliza, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni ipi thamani yake?” Mtume (saw) akasema: **أن تضرب به وجوه العدو حتى ينحني** **“Ni kukata kwa kwao nyuso za adui mpaka upinde.”** Basi Abu Dujana akasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, nitauchukua kwa thamani hiyo. Kwa hiyo, akapewa upanga huo.

Je, majeshi ya Pakistan na Iran yamewapa askari wao na silaha zao haki yake kamili? Majeshi yao ni miongoni mwa majeshi yenye nguvu zaidi duniani, achilia mbali Ulimwengu wa Kiislamu. Ilhali, viongozi wasaliti wametumia mifumo ya zana na silaha za Ummah kinyume na alivyoamrisha Mtume (saw). Kwa hakika, tunawaona wakizionyeshwa ima kwa ajili ya fahari ya kitaifa, au kutumika kuwaunga mkono maadui wa Waislamu, chini ya bendera ya kupambana na ugaidi. Msimamo kama huo uko chini ya hadhi ya dola hizo zenye nguvu za Waislamu. Historia tukufu ya Kiislamu ni ushahidi wa ukweli kwamba dola ya Kiislamu siku zote imekuwa ikibadilisha mfumo wa dunia. Hata hivyo, viongozi hawa wawili duni wa dola hizi mbili kubwa za Kiislamu wanaunga mkono mfumo mbovu wa kimataifa, na dola kuu za kikoloni zinazonufaika nao.

Umefika wakati sasa kwa wenye uwezo na ujasiri kuwaondoa viongozi wa aina hii ambao hawastahili kuwa katika nafasi ya kuongoza majeshi haya yenye nguvu. Ni wakati sasa wa kuondoa nembo na miundo ya dola za kitaifa, na wote wanaozitetea, kwani ndizo zinazoimarisha mfumo wa kimataifa na udhibiti wake. Wakati uwewadia sasa wa mashujaa na wajasiri kujitokeza kuunga mkono kusimamishwa kwa Khilafah

***Endelea... UK 8***

kwa Njia ya Utume. Dola ambayo Mtume Muhammad (saw) alitabiri kurudi kwake. Ni dola itakayorudisha heshima na hadhi inayostahiki Uislamu na Waislamu.

Amesema Mwenyezi Mungu (swt),

يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ ٱلْأَمْرِ مِن شَىْءٍ قُلْ إِنَّ ٱلْأَمْرَ كُلَّهُۥ لِلَّهِ يُخْفُونَ فِىٓ أَنفُسِهِم مَّا
لَا يُبْدُونَ لَكَ يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ ٱلْأَمْرِ شَىْءٌ مَّا قُتِلْنَا هَـٰهُنَا قُل لَّوْ كُنتُمْ فِى
بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ ٱلَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ ٱلْقَتْلُ إِلَىٰ مَضَاجِعِهِمْ وَلِيَبْتَلِىَ ٱللَّهُ مَا فِى صُدُورِكُمْ
وَلِيُمَحِّصَ مَا فِى قُلُوبِكُمْ وَٱللَّهُ عَلِيمٌۢ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ

**“Wakisema: Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili? Sema: Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Wanaficha katika nafsi zao wasiyo kubainishia. Wanasema: Lau ingelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusinge uliwa hapa. Sema: Hata mngeli kuwa majumbani mwenu, basi wangeli toka walio andikiwa kufa, wakenda mahali pao pa kuangukia wafe.(Haya ni hivyo) ili Mwenyezi Mungu ayajaribu yaliyomo vifuani mwenu, na asafishe yaliyomo nyoyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo vifuani.”** [Aali-Imran:154].

**#ArmiesToAqsa**

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Muhannad Mujtaba – Wilayah Pakistan**

# Enyi Waislamu: Mnaona Jinai za Mayahudi kwenye Kivuko cha Rafah, Gaza na kwa hakika Palestina yote.

# Na Watawala Hawapeleki Jeshi kwa ajili ya Kunusuru; Badala yake Wanapuuza Mistari yao Mekundu! Wameridhika na Upatanishi wa Marekani na Wafuasi wake!

**Enyi Waislamu:** Inatosha sasa. Ukatili unaofanywa na Mayahudi kwa watu, miti na mawe hauhesabiki! Sasa wanavamia kivuko cha Rafah, ambacho utawala wa Misri ulikichulia kuwa mstari mwekundu ambao haungekaa kimya kuhusu uvamizi dhidi yake. Lakini wekundu iligeuka kijani baada ya Mayahudi kuikalia kimabavu na utawala wa Misri kuridhika na maandamano pekee!! (Al Jazeera Breaking News,12/5/2024 - Associated Press, ikimnukuu afisa mmoja mkuu wa Misri: Misri iliwasilisha kulaani Tel Aviv, Washington, na serikali za Ulaya kuhusu shambulizi la Rafah). Al-Arabiya Al-Hadath ilikuwa imechapisha mnamo tarehe 7 Mei 2024: (Meja Jenerali Ali Hefzy, Waziri Msaidizi wa Vikosi vya Ulinzi vya zamani vya Misri, katika taarifa za kipekee kwa Al-Arabiya.net na Al-Hadath.net, zilisema kuwa mhimili wa Philadelphia ni eneo la usalama la Palestina kati ya Misri na Ukanda wa Gaza, na kusisitiza kwamba vikosi vya silaha vinalinda mipaka ya Misri kwa usalama mkubwa, na hakuna vikosi vya "Israel" vinavyoweza kukaribia kwa sababu ni mstari mwekundu. Jeshi la "Israel" limetangaza, leo, Jumanne, kwamba limechukua udhibiti kamili wa upande wa Palestina wa kivuko cha ardhi cha Rafah kinachotenganisha Ukanda wa Gaza na eneo la Misri, katika operesheni ya kijeshi ambayo ilianza jana. Magari ya kijeshi ya "Israel" yaliingia katika mhimili wa Philadelphia kwa mara ya kwanza tangu 2005, pia, moshi mkubwa uliongezeka katika eneo karibu na kivuko cha Rafah kati ya Ukanda wa Gaza na Misri huku "Israel" ikizidisha kampeni zake za kushambulia kwa mizinga, leo, Jumanne).

**Enyi Waislamu:**

Inasikitisha kwamba Magharibi, hususan Marekani, zinaongoza watawala katika nchi za Waislamu na kuelekeza nguvu zake katika nchi zinazolizunguka umbile la Kiyahudi, kwani haitaki majeshi yao yaingilie kati. Inatangaza hili kwa kusema: "Msipanue vita"! Inafahamu udhaifu wa umbile hili, kwani uvamizi wake umepita takribani miezi minane bila kufikia malengo yake, japo kinacholikabili ni kundi la waumini ambao ni wachache kwa idadi na vifaa. Kwa hivyo, vipi ikiwa majeshi ya Waislamu yangeingilia kati, au wale tu walio karibu na Palestina? Hili ndilo linaloisumbua Marekani... Hivyo basi, maafisa wake wanazunguka katika eneo hili kuzuia majeshi ya Waislamu kuwanusuru wananchi wa Palestina kwa kuwatia shinikizo watawala wa majeshi hayo, au hata bila ya kuwatia shinikizo! Maana wametelekeza ukombozi wa Palestina kutoka kwa uvamizi wa Kiyahudi tangu 1948 na sio kuanzia leo tu!! Yeyote anayechunguza ziara za maafisa wa Magharibi, haswa Wamarekani, ataona kuwa kwa lengo hili. Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Blinken huwa hatoki kabisa katika eneo hilo. Marekani haikuridhika na hilo, lakini ilimtuma mkuu wake wa ujasusi, William Burns, kuzuru eneo hilo kwa siku kadhaa, akielekeza ziara yake katika utawala wa Misri na umbile la Kiyahudi, hata kama alikuwa anakaa kati yao nchini Qatar. Hata hivyo, msisitizo ulikuwa katika kudhibiti uhusiano kati ya utawala wa Misri na umbile la Kiyahudi, hasa katika suala la Rafah. Hii inafanya kile Al-Arabi Al-Jadeed

***Endelea... UK 9***

ilichochapishwa mnamo tarehe 8/5/2024 kuwa na kipengele kinachostahili kuzingatiwa:

(...Vyanzo vya kibinafsi vilifichua kwa Al-Araby Al-Jadeed kwamba uvamizi wa Rafah na kuwasili kwa gari za jeshi la "Israel" hadi mhimili wa Filadelfia, na hata kwenye lango la Misri la kivuko cha Rafah kutoka upande wa Palestina, zilikuja baada ya upande wa Misri kujulishwa juu yake, na kwa uratibu kamili wa Marekani... Chanzo hicho kilisema, “Mkurugenzi wa CIA William Burns alipanga operesheni hiyo na mkuu wa Mossad David Barnea, huku maongezi ya simu yakifanyika kati yake na Netanyahu, wakati ambapo alithibitisha hali ndogo ya operesheni hiyo.").

Kisha Marekani ilichochea kile ambacho baadhi ya watawala na vyombo kadhaa vya habari vilipongeza, yaani kwamba kulikuwa na mzozo kati ya Marekani na umbile Kiyahudi, na kwamba matumizi yake ya silaha za Marekani yalikuwa ni kinyume cha sheria. Blinken alisema hayo, lakini kwa njia ya kupindisha, ya kuzunguka, na ya udanganyifu, na haifichiki kwa wale wenye uelewa, kama ilivyoelezwa katika ripoti aliyowasilisha kwa bunge la Congress:

[Gazeti la Al-Khaleej: 11/5/2024 Washington - (AFP):

(Ripoti iliyosubiriwa kwa muda mrefu ya Wizara ya Mambo ya Nje mnamo siku ya Ijumaa ilisema kwamba “Israel” huenda ilikiuka kanuni za sheria za kimataifa katika matumizi yake ya silaha za Marekani **lakini haikupata ushahidi wa kutosha kuzuia shehena.**) Ripoti hiyo ilisema, (Ilitathmini kwa busara kwamba “Israel” “ilitumia silaha kwa njia zisizopatana na sheria za kimataifa za kibinadamu,” **lakini Marekani “haikuweza kufikia mahitimisho madhubuti....”** Ripoti hiyo ilisema kwamba (huku Marekani ikiamini kwamba “Israel” imechangia maafa yanayoendelea ya kibinadamu kwa njia ya "vitendo au kutotenda" kwake, **haihitimishi kuwa mamlaka za "Israel" kwa makusudi "imepiga marufuku au kuzuia" utoaji na uhamishaji wa msaada huu ... nk.)]** Ni wazi kwamba inabadilisha maneno ya kulaani na si kutolaani kwa wakati huo huo! Kwa kujali kuwaunga mkono Mayahudi, na kuwahadaa watawala katika nchi za Waislamu, na hata bila ya hadaa, wana ufahamu! Hii ni kuonyesha watu kana kwamba Marekani iko katika mzozo na umbile la Kiyahudi!

**Enyi Waislamu:**

Balaa iko kwa watawala hawa ambao wako katika kuhudumia makafiri wakoloni, hasa Marekani. Wanasema kile inachosema na kufanya kile wanachotaka. Wanashuhudia miili ya mashahidi kwa macho yao wenyewe, wanasikia mayowe ya watoto kwa masikio yao, na wanaona kuhama kwa watu na watoto wao na wanawake katika matukio ya kuvunja nyoyo. Watawala wameshuhudia yote haya. Yamefikia masikio na macho yao, lakini hayakuathiri uungwana wa Al-Mu'tasim (kivitendo)! Wamezuia majeshi yasiwanusuru ndugu zao huko Gaza Hashim. Badala yake, wamesimama na kutazama kile kilichokuwa kikitendeka, wakiwahesabu mashahidi na kuwaita “wafu” kwenye vyombo vyao vya habari. Walio bora zaidi miongoni mwao ni wale wanaopatanisha, kana kwamba ni kundi lisilofungamana na upande wowote kati ya umbile la Kiyahudi, adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Waislamu wa Gaza wanaoshambuliwa katika kila shubiri ya Ukanda wa Gaza!

**Enyi Askari katika Majeshi ya Waislamu:**

Kungojea amri kutoka kwa watawala kupigana na Mayahudi na kuikomboa Ardhi Iliyobarikiwa ni sawa na mtu anayenyoosha mikono yake kwenye maji [kutoka mbali, akiyaita] ili yafikie kinywa chake, lakini hayatafika. Basi anzisheni harakati, nyinyi wenyewe, na Mwenyezi Mungu yu pamoja nanyi na Ummah utawafuata... Bila shaka mnasikia na kuona jinsi adui yenu anavyoushambulia kwa mabomu Ukanda wa Gaza ardhini, baharini na angani ili kuugeuza kuwa ardhi iliyoungua... kwa hiyo munashindwaje kuwanusuru ndugu zenu au kupigana?!

**Enyi Askari katika Majeshi ya Waislamu:**

Je! hakuna miongoni mwenu mtu mwenye hekima? Hususan katika ardhi ya Kinana (Misri) na Ash-Sham, atakayewaongoza askari na majeshi mengine yamfuate, wakipiga Takbira na Umma ukipiga nyuma yao katika ushindi wa Mwenyezi Mungu (swt).

**إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ**

**“Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi.”** [Ghafir: 51].

Imetosha sasa, Enyi Majeshi! Hakuna udhuru uliosalia kwa mwenye kutoa udhuru na hakuna udhuru kwa mwenye kulaani tu. Haitoshi kwenu kukaza meno yenu kwa hasira dhidi ya

**قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ**

**“Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini.”** [At-Tawbah: 14].

**H. 5 Dhu al-Qi'dah 1445** **Hizb-ut-Tahrir**
**M. : Jumatatu, 13 Mei 2024**

# Kuzungumza Neno la Haki kwa Sauti Kubwa

**Swali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakatuh

Nina swali:

Surah Yunus ayah 90: **[فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ] "na Firauni na askari wake wakawafuatia"** na Surat Taha ayah 78: **[فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ] "Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake"**

Je, hii ina maana kwamba amri ya mtawala na kitendo cha mtawala ni kitu kimoja, ili tunaseme kuwa kusimama kinyume na amri zake ni sawa na kusimama kinyume na matendo yake, tukimaanisha kwamba tunaseme neno la haki mbele ya polisi wake au wasaidizi wake, kama kuzungumza mbele yake? أَفْضَلُ الْجِهَادِ كَلِمَةُ حَقٍّ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ **"Jihad bora ni kusema neno la haki mbele ya mtawala jeuri"**. Shukran.

Una haki ya kubadilisha mpangilio wa maneno wa swali hili, na Mwenyezi Mungu akulipe kheri.

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullahi Wa Barakatuh

Kwanza: kuhusiana na ayah mbili ulizozitaja katika swali hili, ambazo ni katika yale ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Surah Yunus, ayah 90:

وَجَاوَزْنَا بِبَنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ بَغْياً وَعَدْواً

**"Tukawavusha bahari Wana wa Israili, na Firauni na askari wake wakawafuatia kwa dhulma na uadui"**, na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema katika Surat Taha, ayah 78:

فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ فَغَشِيَهُمْ مِنَ الْيَمِّ مَا غَشِيَهُمْ **"Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake. Basi kiliwafudikiza humo baharini kilicho wafudikiza!"** Ni kana kwamba unabainisha tofauti katika maana inayotokana na matumizi ya herufi الواو na herufi الباء katika maneno (askari wake), kama anavyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya ya kwanza: فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ **"na Firauni na askari wake wakawafuatia"**, huku Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema katika ayah ya pili:

فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ **"Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake"**. Maana ya "akawafuata" ni kwamba aliwafuata na akawafikia, kwa mujibu wa yale yaliyotajwa katika vitabu vya Tafsiri.

Lakini ayah ya kwanza فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ **"Firauni na askari wake"**, Kwa mujibu wa lugha, inafahamika kuwa Firauni alikuwa miongoni mwa waliowafuata, ikimaanisha kuwa kumfuata Musa, amani iwe juu yake, na Wana wa Israili (Bani Israil) wanajumuisha Firauni, Mwenyezi Mungu amlaani, na alikuwa miongoni mwa watu wale waliowafuata na kuwafikia. Hii ni kwa sababu الواو katika neno (na askari wake) hapa inaashiria kushiriki, yaani kushiriki kwa Firauni na askari wake katika kuwatafuta Wana wa Israili (Bani Israil).

Ama ayah ya pili: فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ **"Firauni pamoja na majeshi yake"**. Inaweza kueleweka kutokana nayo kwa mujibu wa lugha kwamba Firauni alishiriki pamoja na askari wake na mwenzao katika kuwasaka, lakini pia inaweza kueleweka kutokana nayo kwa mujibu wa lugha kwamba Firauni hakushiriki pamoja na askari wake na hakutoka pamoja nao, bali alitafuta tu msaada kutoka kwao katika kuwasaka, na hiyo ni kwa sababu neno "ba" katika lugha linaonyesha uandamani na usaidizi. Kwa hiyo neno (pamoja na askari wake) katika ayah hiyo linaweza kutumika kama lugha ya kuambatana, ikimaanisha kwamba Firauni aliandamana na askari wake katika kuwafuata Bani Israil, na pia inaweza kuchukuliwa kuwa ni kutafuta msaada, **ikimaanisha inaweza kuwa alikuwa pamoja nao, na inaweza kuwa alitafuta msaada kutoka kwa askari wake ili kuwafuatilia bila ya kushiriki nao,** maana yake ni kwamba waliowafuata ni askari wa Firauni bila ya Firauni mwenyewe.

**Utambulisho wa mojawapo ya maana hizi mbili (usindikizaji au usaidizi) unadhihirika kutokana na mchanganyiko wa aya hizo mbili:**

Ayah ya kwanza ina maana moja katika lugha. Na ni kwamba Firauni, Mwenyezi Mungu amlaani, aliungana nao, yaani, masahaba zake, katika kumkamata Musa (as). Maana ya Aya ya pili yaelekea ni katika lugha ya kuambatanisha, maana yake alifuatana nao katika kumkamata Musa, amani iwe juu yake, na pia yawezekana aliomba msaada, maana yake aliomba msaada kwa askari wake ili kumkamata Musa (as) bila ya Firauni kuwafuata, Mwenyezi Mungu amlaani katika hilo. Kwa sababu maana ya Aya hizo mbili hazipingani, maana ya kuziunganisha Aya hizo mbili ni kwamba

***Endelea... UK 11***

Firauni alikuwa na jeshi lake katika kumfuata Musa (as). Yaani الباء katika “pamoja na askari wake” hapa inaashiria maana ya kuandamana, kumaanisha kwamba alikuwa na jeshi lake katika kumfuata Musa, amani iwe juu yake. Hii ni kuhusiana na maana ya Aya hizo mbili.

**Pili: Ama Hadithi tukufu** iliyotajwa katika swali hili, imepokewa na Al-Tirmidhi katika Sunan yake kutoka kwa Abu Said Al-Khudri kwamba Mtume (saw) amesema:

إِنَّ مِنْ أَعْظَمِ الْجِهَادِ كَلِمَةَ عَدْلٍ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ **"Hakika, miongoni mwa Jihad kubwa ni kusema neno la haki mbele mtawala jeuri"**. Abu Issa amesema, na katika sura hii kutoka kwa Abu Umamah, na hii hadith hasan ghareeb kwa mtazamo wake. Imetajwa katika Al-Mu’jam Al-Kabir ya Al-Tabarani kutoka kwa Abu Umamah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

أَحَبُّ الْجِهَادِ إِلَى اللهِ كَلِمَةُ حَقٍّ تُقَالُ لِإِمَامٍ جَائِرٍ **“Jihad inayopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni kusema neno la kweli kwa Imam jeuri”**. Katika riwaya nyengine ya Al-Tabarani kutoka kwa Abu Umamah, kwamba mtu mmoja alisema katika Jamarat: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni jihad gani iliyo bora? Akasema:

أَفْضَلُ الْجِهَادِ كَلِمَةُ حَقٍّ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ **“Jihad iliyo bora kabisa ni kusema neno la kweli mbele ya mtawala jeuri.”** Yafuatayo yametajwa katika kitabu cha Aoun Al-Ma'boud katika kuielezea Hadithi hii: [... Kutoka kwa Abu Said Al-Khudri, ambaye amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: Jihad bora kabisa. ni neno la uadilifu kwa mtawala dhalimu. Swahaba wa Awn al-Ma'boud alisema:

(Jihad iliyo bora kabisa): Yaani, mojawapo ya bora zaidi, kama inavyo thibitishwa katika riwaya ya Al-Tirmidhi: Hakika, miongoni mwa jihadi kubwa kabisa (Neno la uadilifu) Na katika riwaya ya Ibn Majah kuna neno haki, na linalokusudiwa na neno hilo ni lile linaloamrisha mema au kukataza maovu, sawa iwe ni neno au maana yake, maandishi na mfano wa hayo.

(Kwa mtawala jeuri): Yaani dhalimu. Hakika hii imekuwa ni jihad bora kabisa, kwa sababu anayepigana dhidi ya adui anasitasita baina ya matumaini na khofu, bila kujua atashinda au atashindwa.

Mwenye mamlaka amedhulumiwa mkononi mwake, hivyo iwapo atasema ukweli na kumuamrisha M’aruf (mema), amefichua uharibifu na analenga kuangamia yeye mwenyewe. Hii inakuwa aina bora ya jihad kwa ajili ya kuishinda hofu, kama Al-Khattabī na wengineo walivyosema. (Au mtawala dhalimu (Amiri)): Inaonekana kwamba ni shaka kutoka kwa msimulizi.].

Kutokana na Hadith hii tukufu inaweza kufahamika kwamba jihad iliyo bora zaidi ni kusema neno la ukweli mbele ya sultan dhalimu, sio mbele ya wafuasi wake. Kinachomaanishwa na sultan dhalimu ni mwana mtawala dhalimu, awe rais, mfalme, waziri mkuu, au gavana. Ni lazima awe na mamlaka na utawala ili upendeleo huu utolewe katika kusema ukweli mbele yake.

Lakini hii haimaanishi kwamba hakuna wema katika kusema neno la ukweli mbele ya wafuasi wa mtawala dhalimu. Kusema neno la kweli siku zote ni jambo la kheri na la jema. Hata hivyo, faida maalum ambayo Mtume (saw) aliitaja katika Hadith tunayozingatia ni upendeleo unaohusiana na mwenye mamlaka, yaani, mtawala mwenyewe. Kwa sababu ya umuhimu wa kusema neno la ukweli mbele yake na hatari, ujasiri, na nguvu inayohusika, kama baadhi ya wafasiri wa Hadith walivyotaja:

**[... Al-Khattabi amesema: Hakika hiyo ikawa ndio jihad bora kabisa; Kwa sababu anayepigana na adui husitasita baina ya matumaini na hofu, bila kujua atashinda au atashindwa. Mwenye mamlaka amedhulumiwa mkononi mwake, basi iwapo atasema kweli na akamuamrisha M'aruf (mema), amefichuliwa uharibifu, na amejiweka kwenye maangamivu, na hii imekuwa ni aina bora za jihad kwa ajili ya kuishinda hofu. Al-Muzher amesema: Lakini ilikuwa bora zaidi kwa sababu dhulma ya Sultan inamhusu kila mtu chini ya utawala wake, na ni umati mkubwa. Kwa hivyo, ikiwa atakataza dhulma, basi ataleta manufaa kwa watu wengi zaidi ya kumuua kafiri...].**

Mazungumzo yote ni juu ya mtawala dhalimu mwenyewe, sio juu ya wafuasi wake, wasaidizi, na askari.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**


#طوفان_الأقصى
#الجيوش_إلى_الأقصى
#ArmiesToAqsa
#AksaTufanı
#OrdularAksaya
#Aqsa_calls_armies
#AqsaCallsArmies
#الأقصى_يستصرخ_الجيوش